

# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



## MNADA WA HADHARA

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi wote kuwa, kutakuwa na mnada wa hadhara kwa ajili ya kukodisha eneo la **Bustani ya Mapumziko ya Chinangali (Chinangali Recreational Park)** iliyoko jirani na Uwanja wa Ndege Jijini Dodoma.

Mnada utafanyika **Siku ya Jumamosi tarehe 21/11/2020 na mahali ni hapo hapo eneo la bustani, muda ni kuanzia Saa 3:00 asubuhi.**

### **MASHARTI YA MNADA KWA AJILI YA UKODISHAJI WA BUSTANI YA MAPUMZIKO YA CHINANGALI**

1. Kila mshiriki wa mnada lazima ajisajili kwenye rejista ya mnada.
2. Kila mshiriki wa mnada huo atatakiwa kulipa fedha taslim Tshs 2,000,000 (milioni mbili) tu kabla ya mnada kuanza ikiwa ni dhamana na atakayeshindwa atarudishiwa pesa yake hapo hapo baada ya mnada kumalizika.
3. Mnada utakuwa ni wa hadhara na jambo lolote linalohusiana litaongelewa eneo hilo hilo la mnada kwa uwazi.
4. Mwombaji atakayetoa pendekezo la kodi kubwa zaidi ndiye atakayepatiwa nafasi ya kuendesha eneo hilo.

5. Mwombaji atakayefanikiwa kushinda mnada huo atawajibika kulipa kodi zote za Serikali kwa mujibu wa sheria za nchi.
6. Mshindi wa mnada atatakiwa kulipa asilimia 25 ya kodi ya pango ya kipindi cha miezi mitatu siku ya mnada, na kumalizia asilimia 75 kabla ya kuanza kuendesha bustani hiyo kama dhamana (mshindi anaweza kulipa kiasi chote siku hiyo hiyo).
7. Mnada utafanyika tarehe 21/11/2020 katika eneo la Bustani ya Mapumziko ya Chinangali (Chinangali Recreational Park) kuanzia saa tatu (3.00) kamili asubuhi.

### **MAELEZO KUHUSU BUSTANI YA MAPUMZIKO YA CHINANGALI (CHINANGALI RECREATIONAL PARK)**

- Eneo lote la bustani limepimwa na lina ukubwa kiasi cha ekari 12.3 (Mita za mraba 60,270).
- Eneo la michezo ya watoto lina Mita za mraba 1,564.
- Njia za kutembea ndani ya bustani zina urefu wa Kilometa 1.25 (Mita 1,250).
- Kuna viwanja vya michezo mbalimbali kama vile mpira wa Kikapu, mpira wa wavu, mpira wa tenis, mpira wa mikono.
- Kuna mabwawa ya kuogelea kwa wakubwa na watoto.
- Kuna eneo la mazoezi ya mwili (**gym**) lenye ukubwa wa mita za mraba 144 (ofisi, stoo, vyoo na vyumba vya kubadilishia nguo kwa wanaume na wanawake).
- Kuna Vioski vinne vya huduma za Chakula na Vinywaji.
- Kuna Jukwaa la burudani na matamasha.
- Kuna vyoo vya kisasa na vyumba vya kubadilishia nguo kwa wakubwa, watoto na walemauvu.

- Kuna sanamu za wanyama mbalimbali (Tembo, Faru, Nyati, Twiga, Simba na Swala)
- Kuna eneo la maegesho ya magari yapatayo 108 lenye ukubwa wa mita za mraba 3,431
- Kuna vivutio mbalimbali kama vile 'Water Fountain', Taa za aina na rangi mbalimbali, miti ya matunda na vivuli.
- Kuna ofisi za utawala.
- Kuna kisima cha maji safi ya uhakika.
- Kuna 'standby generator' kwa tahadhari umeme unapokatika.
- Kuna kamera za usalama (CCTV camera).
- Eneo lote limezungukwa na uzio.

Tangazo hili limetolewa na:



JOSEPH C. MAFURU  
**MKURUGENZI WA JIJI**  
**DODOMA**